

Kuongeza Mtegemezi kwa usaidizi wako wa utafutaji kimbilio



scottish
refugee
council

Januari 2009

Adding an adult dependant - Swahili

Iwapo kwa sasa unapokea usaidizi wa kutafutaji kimbilio (iliyojulikana kama NASS) kutoka kwa Ofisi ya Nyumbani Wakala wa Mipaka ya Uingereza) na mume wako, mke au mwenzi ameungana nawe Uskoti; inawezekana kuwaongeza kama mtegemezi mzima kwa usaidizi unaopokea.



Fahamu kuwa kuongeza mtegemezi kwa usaidizi wako hakumaanishi kuwa wameongezwa kwa dai lako la utafutaji kimbilio. Tungekushauri kuwa ujadiliane kuhusu jambo hili na mwakilishi wako wa kisheria, kwani mabadiliko katika hali yako ya jamii **yanaweza** kuathiri kesi yako ya uhamiaji.

Kijitabu hiki kinaweza kuongezwa kama mtegemezi mkubwa kwa usaidizi wa utafutaji kimbilio unaopokea kutoka kwa Ofisi ya Nyumbani, ni nyaraka gani zinahitajika ili kusaidia ombi lako na jinsi tunavyoweza kusaidia.

Ni nani anaweza kuongezwa kwenye usaidizi wako kama mtegemezi?

Iwapo unajaribu kuongeza mtegemezi mzima kwa usaidizi wako wa utafutaji kimbilio, ni **lazima** wajulikane na Ofisi ya Nyumbani. Iwapo hawajawalisiana na Ofisi ya Nyumbani, au hujawahi kudai kimbilio katika Uingereza, lazima uongee na mwakilishi wa kisheria kabla ya kuchukua hatua zaidi.

Ili kuongezwa kwa usaidizi wa utafutaji kimbilio unaopokea kutoka kwa Ofisi ya Nyumbani, mwenzi wako lazima afikie moja ya mambo yaliyo hapa chini: Lazima awe:

- Ameolewa na wewe; **au**
- Ameishi na wewe kama wenzi ambao hawajaoana katika Uingereza kwa angalau miaka mitatu iliyopita; **au**
- Amekuwa mtegemezi katika dai lako la utafutaji kimbilio kabla ya kukataliwa.

Ni nyaraka gani ninafaa kutoa ili kuongeza mwenzi wangu kama mtegemezi?

Illi kuongeza mtegemezi mkubwa kwa mipango yako ya usaidizi, lazima utoe ombi lililoandikwa kwa Ofisi ya Nyumbani ambayo imetiwa saina na wewe na mwenzi wako. Lazima pia utoe ushahidi wa uhusiano weny. Ushahidi unaokubalika ni pamoja na:

- Hati yako ya kuolewa
- Hati ya mtoto wako ya kuzaliwa inayoonyesha mke, mume au mwenzi wako kama mzazi

Iwapo hujaolewa **au** huna hati yako ya kuolewa tena au hati ya kuzaliwa ya mtoto wako, unaweza kutoa:

- Ushahidi ulioandikwa ambao ulimtaja mwenzi wako kwenye mahojiano na Ofisi ya Nyumbani au katika ombi lako la usaidizi wa utafutaji kimbilio.
- Barua za hati za matumizi zilizo na jina zenu zote zinazoonyeshwa na anwani zinazofanana
- Nakala za dai lako mpya la utafutaji kimbilio au Hojaji ya Urithi ambayo inaeleza wategemezi na inathibitisha uhusiano wenu.

Tunaweza kukusaidia vipi?

Tunaweza kukusaidia na mwenzi wako ili kukamilisha ombi lako la kwanza lililoandikwa kwa Ofisi ya Nyumbani. Tafadhali fahamu kuwa ni juu yetu kuongea nawe na mwenzi wako kabla ya kuwasilisha ombi hilo.

Inaweza kuchukua muda wa wiki mbili kwa Ofisi ya Nyumbani kutengeneza ombi lako. Ofisi ya Nyumbani itakuandikia moja kwa moja ili kukueleza kuhusu uamuzi wao. Iwapo hujapokea fomu yoyote ya mawasiliano kutoka kwa Ofisi ya Nyumbani baada ya wiki mbili, tafadhali wasiliana nasi.

Iwapo unahitaji kusahihisha tondoti zako za kuwasiliana au utushauri kuhusu mabadiliko yoyote ya hali yako, unaweza kutupigia **simu yetu ya bure: 0800 085 6087** na uongee na mfanyakazi wa zamu wa kesi yako.

Ni nini hufanyika iwapo ombi lako limekataliwa?

Iwapo ombi lako limekataliwa, tunaweza kukusaidia kukata rufaa kwa shirika huru linaloitwa Baraza la Usaidizi wa Utafutaji Kimbilio (AST). Tondoti za rufaa yako zitalingana na sababu ambazo Ofisi ya Nyumbani itatoa kwa kukataa usaidizi.

Unaweza kuhudhuria rufaa hiyo katika London iwapo ungependa kutoa kesi yako kwa baraza hili . Iwapo utaeleza Ofisi ya Nyumbani kabla kuwa ungependa kuhudhuria, wanaweza kugharamia safari yako.